TANGAZO LA SERIKALI NA. 83 la tarehe 17/2/2023

SHERIA YA MIPANGO MIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetolewa Chini ya Kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KWEDIZINGA, TAULA NA UGWENO YA MWAKA

Jina

1. Amri hii itaitwa Amri ya Kupanga Eneo La Kwedizinga, Taula na Ugweno ya Mwaka 2023.

Kutangaza eneo la Upangaji
Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Kuandaa Mipango ya jumla na ya kina.

3. Mipango ya Jumla na ya Kina katika eneo lililoainishwa katika Jedwali itaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Handeni.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo: -

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba VTB 93 yenye majira - nukta 450621MS, 9397798KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa umbali wa kilomita 9.5 katika uelekeo wa 180° 12’ 40’’ hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji yenye majira - nukta 450546MS, 9407297KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 2.3 katika uelekeo wa 236° 27’ 10’’ hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba NP1 yenye majira - nukta 448559MS, 9405978KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 11.3 katika uelekeo wa 85° 34’ 09’’hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba GY412 yenye majira - nukta 437196MS, 9405067KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 6.9 katika uelekeo wa 165° 02’ 52’’hadi kwenye alama ya mpaka wa upimaji namba NP yenye majira - nukta 437976MS, 9398148KZ; hadi ulipoanzia”.

Dodoma,
6 February, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*